# KINGA

"Wanaume na Kondomu wakati wa VVU na UKIMWI"

Kitabu cha Msaidizi

© Sonke Gender Justice Network

**NDANI YA GAMBA LA JUU**

USEMI KATIKA PICHA TOKA FILAMU
*“Kwa nini, kama kondomu zinapatikana, VVU vinaendelea kuenea Afrika?”* - *“UKIMWI haujafasiriwa vizuri kwa watu, na kwamba ukitumia kinga utaweza kuuzuia” …*

*“Nimepoteza dada, ndugu, mume kwa sababu ya kutojua. Kama wangefahamu kuhusu kondomu wangekua bado wapo hapa.”*

*“Hebu tusijidanganye wenyewe… Nususi ya mambo ni kwamba watu wanafanya mapenzi.”*

*“Wakati unakunywa vileo hauwezi kuvaa kondomu vizuri, tayari umepata kizunguzungu na unasema ‘Mimi ni mwanaume, UKIMWI haupo’ – na mwishoni utafariki peke yako.”*

*“Aibu ndiyo imekatilia watu wetu mbali nasi.”*

*“Asilimia kubwa ya wenye kuathirika sasa ni watu wenye kufunga ndoa”.*

**YALIYOMO**


**1. Shabaha ya kinga**

**2. Kwa nini kondomu?**

**3. Siyo tu Ujumbe na Hakika, bali Majadiliano na mazungumzo**

**4. Njia za kutumia DVD**

**5. Mashauri madogo kwa Wasaidizi**

**6. Kujiandaa kwa ajili ya majadiliano baada ya filamu**

**7. Masuala itajadiliwa kuhusu filamu nzima**

**8. Masuala itajadiliwa: Ukurasa wa Afrika ya Kusini**

**9. Masuala itajadiliwa: Ukurasa wa KENYA**

**10. Masuala itajadiliwa: Ukurasa wa SIERRA LEONE**

**11. Maneno itajadiliwa kuhusu ‘maziada’ mafupi**

**12. Nyenzo zingine na Ukurasa wa Maarifa katika mtandao**

**Shabaha ya kinga**

DVD hii, pamoja na Kitabu chake cha Msaidizi, ni nyenzo za kuthibitisha kupanuka kwa majadiliano kuhusu kondom katika kazi yako ya uzuiaji wa UKIMWI pamoja na vijana na watu wazima. Kitabu hiki kinaweza kikakusaidia katika maandalizi ya majadiliano kuhusu filamu. Tovuti ya filamu hutoa habari zaidi kuhusiana na kondomu pia huchunguza kwa kinaganaga baadhi ya masuala yenye kutiwa mkazo humu.

**KINGA** si filamu ya hakika na nasaha. Waweza na inabidi upange hizi, zenye kurekebishwa na miuktadha pamoja na haja za umma. Bali ni filamu yenye kutungwa kwa ajili ya kusisimua katika nchi za Sub-saharan Afrika kuenea kwa majadiliano kuhusu mtazamo na usalama wa vijana na wanaume katika wakati ambao maisha ya mamilioni ya watu imeendelea kuathiriwa na VVU na UKIMWI.

Filamu inatia mkazo juu ya masuala na mitihani kuhusu matumizi ya kondom. Watu katika filamu wanasema vitu ambavyo vinaweza kufurahisha au kuhuzunisha, kuchochea makubaliano au ubishi. Lakini kuliko kuepuka mabishano, dhana na mazoea ya maisha ya kweli, uzuiaji wa VVU wapaswa kutoa jibu kuhusu nususi ya mambo, nini wanaume na vijana wanafikiri na KUFANYA. Tunahitaji kutumika tukifikiria nususi ili tupate kuthibitisha uwezekano kwetu  wote wa kufikiri na kutenda kwa usalama kuhusiana VVU.

Kwa kutoa wazo katika nususi ya mambo mbalimbali, vishawishi, kutofahamu, unyamavu na vinyume wanaume wanakusa kuhusu VVU, **KINGA** yaweza kua njia nyepesi kwa kuzungumzia zaidi afya ya ngono na mitihani wanapata mara kwa mara wanapojifunza kujikinga wenyewe.

DVD ina michaguo  kadhaa ya menyu. Oneni YOTE kwanza, halafu chagueni nini itatosha kuhusu mipango yenu. Kitabu cha msaidizi hiki pamoja na linki ya tovuti ya filamu vitakusaidia katika maandalizi ya kuonesha filamu na kuongoza mazungumzo baadaye.

Basi unaweza:

- kuonesha FILAMU NZIMA, ambayo imetunga mitihani kadhaa
- kuangalia  sehemu za filamu kwa kipekee
- na/au kushirikisha ‘MAZIADA’ mafupi yenye kuelekezwa katika vikao vifupi vya baraza kwenye DVD.

**Kwa nini kondomu?**

Kondomu zimekuwa leo njia MOJA TU ya kupunguza zaidi hatari ya kuathirika na VVU wakati wa tendo la ngono au ngono kinyume. Kondomu zinaweza kukinga na MAGONJWA YA ZINAA yenye kusababisha ugumba kwa wanaume na wanawake. Kondomu zinaweza zikakusaidia uepuke maradhi yenye kuhatarisha uzima kutokana na VVU visivyotibiwa – au kuepuka kutumia tiba za nguvu za VVU siku zote za maisha. Kama unaishi na VVU, Kondomu zinawezesha maisha ya ngono mepesi na yenye kuridhisha, umbalimbali na mavune ya VVU mengi au tofauti, au maradhi ya zinaa mengine, unapokua na uhakika wa kupunguka zaidi kwa hatari ya maambukizi kwa mtu mwengine. Kondomu ni 'kifaa cha maisha'.

Kuhusu ngono, unaweza ukaepuka VVU kwa kuacha kufanya mapenzi kabisa kabla ufunge ndoa, na ukiwa na mwenzi wa mapenzi mmoja wa muda mrefu, ulipochunguzwa kama si muathirika wa VVU. Lakini kama umekua na wenzi tofauti, katika sehemu yoyote ya maisha yako – Kama baadhi ya wanaume na wanawake hufanya duniani – unahitaji kinga la kondomu unapojamiiana nao wote. VVU huweza kuwa mwilini bila ishara yoyote kwa miaka mingi. Ni vipimo tu hufunua nani alie na VVU. Vijana na wanaume wengi wanajihatarisha, wakifunga jicho, wanapotumaini, ingawa wanafanya ngono isiyo salama, wao si wenye kuathirika na VVU – Bila kujua ya kwamba magonjwa hii ya zinaa yaweza kusababisha ugumba. Usalama umesuswa na dhana kwamba tendo la ngono huweza kusimamishwa wakati 'hisia imekua sawa', na kwamba kondomu hupotoa hisia/matokeo.

Watu milioni 22.4 wanaishi na VVU katika sub-Saharan Afrika: kila mwaka milioni mbili zaidi wanapata VVU na milioni 1.4 wanafariki kutokana na UKIMWI. Mamilioni ya watoto wamepoteza wazazi. Imani na mila haiwezi ikakomesha mlipuko.

Dawa za ARV zenye kupunguza ukali wa VVU mwilini zinaendelea zaidi kupatikana. Kuwa muathiriwa wa VVU sasa ni hali inaweza kudhibitiwa, ikiruhusu maisha kuendelea kama kawaida, pamoja na ujauzito wenye kukingwa, na bahati kubwa za kutoendelea kwa VVU hadi UKIMWI. Dawa za ARV ni dawa kali ambazo watu wanakunywa kwa kawaida na kila siku **ya baki la maisha ya mtu**. Bila chakula bora, zinaumiza mwili. Wengi bado hawawezi kuzipata. VVU huweza kubadilika na kupata kushinda ukali wa Dawa za ARV zenye kupatikana. Kuepuka kupata (mara tena) maradhi ya VVU huitaji kuchukua hatua kwa haraka zaidi.

Wanaume na vijana wamekosa mara nyingi ufahamu sahihi kuhusiana na VVU, usalama wa ngono, anasa – na matumizi ya kondomu. Ukosefu wetu wa uwezo wa kuepuka maambukizi ya VVU katika na kutoka miili yetu wenyewe huruhusu VVU kusambazwa katika maisha mengi zaidi.

**Siyo tu Ujumbe na Hakika, bali Majadiliano na mazungumzo**

Vijana na wanaume wanaona kondomu mara nyingi zaidi katika kutaniwa, kusikia watu wakisema, hadithi au mashauri ya utawa yenye kuwakatilia mbali – au katika miito ya habari (mara nyingi yenye kuchekesha) au tu katika baraza kuhusu VVU.

Wameshawishiwa na kawaida za kienyeji za kiume, si rahisi wanaume wazungumzie matumizi ya kondomu kwa dhati au kwa kinaganaga pia ni vigumu wapate kushiriki katika majadiliano maarufu yenye kuhusika na afya ya ngono pamoja na ujinsia. Wanaume na vijana wengi wanadhani kwamba ngono ni kitu unafanya, si chakuzungumzia wala kufikiria.

Mambo kama ujumbe wenye kupinga matumizi ya kondomu na kusemasema kwa watu hufika mbali zaidi kushinda matangazo halisi na sahihi kuhusu matumizi sahihi. Wemepoteza moyo wa kutumia kondom, wanaume wengi wanatenda ngono bila kinga. Wanapopata VVU au magonjwa mengine ya zinaa, au wanaposababisha mimba zisizotarajiwa, wanatambua kwamba maisha yao imejikuta katika mambo hawakutaraji na matatizo ambayo kondomu ingezuia.

Kushirikisha wanaume katika mazungumzo inayohusiana na kondomu kunaweza kuchochea fursa zinazohusika na kuepuka katika ngono matokeo mabaya au isiyotarajiwa. Hivyo hatari za kuathirika na VVU zimekuwa wazi zaidi, watu wanaweza kuchagua kukwepa au kudhibiti VVU kwa kuhiari mbinu yenye kuwa salama zaidi kuhusu ngono (bila kuhitaji kondomu) – au kuwa zaidi tayari kufanya tendo lolote la ngono salama kwa kuwa wana ufahamu wa matumizi ya kondomu. Kupitia mojawapo wa njia hizi, uwezo wa wanaume kwa kuhifadhi maisha yao ya ngono miongoni mwa VVU umekuwa imara.

Filamu hii husaidia kwa kuanzisha mazungumzo makuu yenye kuhitajiwa kwa kuhamisha utelezi hadi razini sahihi kuhusiana na uzuiaji (wakati VVU vinaendelea kusambazwa). Inachochea mabishano kwa kutia mkazo juu ya nususi na mitazamo wanaume na vijana wanaweza kupata mara kwa mara. Inakupa mazingira ambayo ndani yake wewe, kama msaidizi, unaweza kukaza vizuri juu ya uzuiaji wa VVU, afya ya ngono na suala za anasa, na mashaka ya wanaume na vijana ambao unatumika nao.

Mazungumzo, mabishano na masuala yenye kuchochewa na maisha na mawazo ya watu katika filamu inatoa nafasi kwa kuzungumzia kwa ajili ya kutia wazi ufahamu kuhusu kodomu na kuthibitisha ufahamu sahihi wa matumizi mazuri ya kondomu. Inatoa nafasi kubwa zaidi kwa kusaidia mwanaume na vijana ili wapate ujuzi wa kawaida unaohitajiwa kuhusiana na matumizi sahihi ya kondomu – na kufanya matumizi ya kondomu kuwa kawaida katika  mahusiano yao. (Tazama 'maziada' mafupi katika DVD kwa kutia mkazo juu ya masuala tunazungumzia hapa).

**Njia za kutumia DVD**

**KINGA** ina sehemu tatu, zimepigwa katika nchi na nafasi tatu tofauti:

**Sehemu ya 1** inatia mkazo juu ya watu katika kilabu ya ndondi jijini Soweto na Johannesburg, Afrika ya Kusini – huko watu wengi zaidi wamepata VVU na wengi wao wameathirika na UKIMWI. George, kocha mkuu, mwenye kujitoa katika mazoezo ya mwili, ujuzi kuhusu kujikabili mwenyewe na afya ya miili ya vijana, anakataa kwa ukaidi kufikiria uzuiaji wa VVU. Moruti, mwenye kujitoa katika kutunza afya ya mwili , pamoja na taji la dunia kama shabaha ya maishai yake, amefanya uzuiaji wa VVU kuwa sehemu ya maisha yake.

**Sehemu ya 2** inaonesha Elkana, Mzee kijijini katika sehemu ya Kenya iliopigwa sana na VVU, ambae familia yake mwenyewe imeathirika na UKIMWI. Anaalika baraza/mkutano wa umma kwenye watu, ambao maisha ya wengi wao ni katika athari ya VVU, wanasema toka mioyo yao wanapozungumzia matumizi ya kinga, desturi na nususi.

**Sehemu ya 3** inatia mkazo juu maaliko ya kushirikisha wavulana katika kuepuka kwa VVU. Maisha ya wavulana wawili katika Sierra Leone imejengwa na kuonyesha kwa ujasiri wa kiume, mabishano kawaida kati ya mashauri ya watu wazima na safari ya vijana kwenye pendekezo, kuendelea kuishi na hatari pamoja na nususi kutokana na ngono isiyo salama wakati wa umaskini na shida baada ya vita.

Katika ‘Maziada’ ine mafupi

- watu wenye kusimamia afya ya wanaume kingono toka nchi mbalimbali za Afrika wanazungumzia kondomu
- Mtu mwenye kuelimisha anajadili na vijana kuhusiana na kondomu
- Taswira zilizo hai zinafasiri jinsi gani (kuto) tumia kondomu kunaweza kuathiri maisha ya mtu
- Mwanasiasa Mwafrika anazungumzia watu na VVU kwa moyo wake wote.

Menyu ya DVD inaweka tayari michaguo hii:

- Onyesha filamu nzima – dakika 110.

- Onyesha mojawapo ya sehemu tatu (takriban dakika 35 kwa kila mmoja). Zinapoonyeshwa katika taratibu hii, sehemu za 1 na za 3 zinashirikisha ziada mfupi (soma juu).

- Tumia mojawapo ya ‘Maziada’ manne mafupi (dakika 2 au 7) kwa kuchochea majadiliano kwa vipindi vifupi zaidi, au kwa kutia mkazo juu ya kufuatilia majadiliano

**Inapowezekana, onyesha filamu <u>nzima</u> katika mkusanyiko mmoja – inakuingiza katika safari, toka jitihada za watu kwa kuthibitisha miili yenye nguvu na afya hadi misimamo, nususi ya mambo na maaliko ya kiume ambayo inaweza kuweka miili ya watu katika hatari kutokana na VVU.**

**Mashauri kidogo kwa Wasaidizi**

**KABLA YA MKASA**

- Fahamu vizuri filamu na ‘Maziada’, masuala inayotokea na mbinu za sasa kuhusu uzuiaji wa VVU.

- Fikiria vizuri *mwenyewe* masuala ya majadiliano. Kuna ripoti kuhusu VVU na matumizi ya kondomu katika tovuti ya filamu (ambazo waweza kuchapa kama machapisho).

- Zaidi unakuwa tayari kwa kuraisisha majadiliano yenye matatizo, vivyo hivyo zaidi mkasa wako utafanikiwa.

- **Chukua mpango kuhusu nini kuonyesha na kujadili –** kama kuonyesha filamu nzima, sehemu moja kwa moja au baadhi ya ‘Maziada’. Tengeneza masuala ya majadiliano ambayo itatosheleza nia yako pamoja na watazamaji fulani wako. Ni ya muhimu kukusanya watazamaji kwa umri?

- **Jua nia yako.** Ufahamu wa mitihani ya uzuiaji? Majadiliano yenye kuwa na yenye kutokana na ufahamu kuhusu kondomu? Badiliko la tabia? Fanya taratibu na fuatilia matengenezo kwa kutimiza shabaha zako.

- **Fanya matengenezo mapema. Chagua nafasi na wakati tayari kwa vijana/wanaume**. Tangaza waziwazi nafasi mkasa utafanyika na utachukua muda gani.

- **Jua vifaa vyako.** Pima KILA MARA seti ya sauti/taswira kabla ya mkasa. Kama unatumia laptop na LCD projector, tafuta kupatikana kwa chanzo cha umeme wenye kuhitajiwa, ma adapters, kabe, na vipaza sauti, kuta mweupe au pazia kwa kuonyesha. Kama unatumia runinga au DVD player, uhakikishe zimechomekwa, zimeunganishwa vizuri.

**Mashauri kidogo kwa Wasaidizi**

**UNAPOONYESHA**

- **Eleza kuhusu filamu**, utaratibu wake – shabaha yake inapokua kuanzisha majadiliano.

- **Tengeneza nafasi nzuri kwa ajili ya majadiliano baadaye** – panga viti kwa mviringo, toa meza zote, anza na michezo au hatua za mwanzo. Tayarisha kila mara chakula au vinywaji.

- **Panga kanuni za msingi pamoja na washiriki -** heshima, kusikia, usiri, hakuna vileo, zima simu ya mkono na kadhalika – kwa kufanya mazingira iwe salama na yenye kuruhusu watu wakaribie.

- **Tumika ukihisi** ushahidi tofauti wa watu**, na rudi nao kwenye majadiliano**.

- **Thibitisha usikivu kwa unyenyekevu.** Kama mtu anahukumu watu katika filamu, akisema ni ‘kosa’ lao, ni ya muhimu kuzungumzia mambo ya jamii (kiuchumi, nguvu za kisiasa, taratibu za jinsia,) kwa kugusa maisha ya watu.

- **Shirikisha kila mmoja. Majadiliano katika jozi za watu au vikundi vidogo yaweza kusaidia hiyo**.

- **Kubali ubishi wenye kujenga**. Uwe tayari kumudu migogoro mibovu au watu wagumu,labda husisha mtu mwenye uzoefu katika kumudu mambo kama haya.

- **Hakiki nini imetosheleza.** Ruhusu wakati wa kutathmini vitendo toka mkutano, fikiria masuala iliotokea, mitihani, masuala yenye kuhitaji mazungumzo siku za mbele. Uchunguzi wa msimamo wa washiriki ungeweza kuelimisha kuhusiana na kazi mbeleni.

**Kujiandaa kwa ajili ya majadiliano baada ya filamu**

Katika ukurasa zijazo kuna masuala kwa kusaidia kutia mkazo juu ya majadiliano baada ya kuona filamu nzima, sehemu moja kwa moja au ‘maziada’. Andaa taratibu ya majadiliano baada ya filamu. **Soma mapema masuala yote na uifanye kuwa aula yenye kutosheleza zaidi kwa ajili ya kikundi chako.**

Ni ya muhimu watu watoe mawazo yao kuhusiana na masuala yenye kusababishwa na filamu. Thibitisha usikilivu na heshima kuhusu maoni tofauti. Wezesha kupata maarifa sahihi yenye kupatikana. Fafanua vitu bila mpango ambavyo watu wanasema katika filamu (k.m. VVU ni hukumu ya mauti; VVU ni suala yenye kuhusisha vijana na vibibi tu; watu ‘wanaeonekana kuwa safi’ hawapo na VVU).

Kondomu zinaweza kutoa tatizo kwa wanaume wa umri wowote. Thibitisha matangazo ya mawazo tofauti kuhusu mitihani ambayo VVU vimetia mbele ya watu na dhima za kondomu katika uzuiaji wa VVU (na magonjwa ya zinaa, ugumba, mimba isiyotarajiwa) na kwa kumudu mapenzi salama zaidi na yenye kutosheleza zaidi kama ni muathirika wa VVU. Kutakuwa watu katika kikundi ambao *wana* au *wata*husika na jambo hii.

Neno watu wanasema si kila mara kionyesho ya vitu ambavyo **wanafanya** hakika katika maisha yao. Fedheha kuhusu kondomu, hadithi na ujumbe wa dhambi juu ya ngona kabla au inje ya ndoa, zinathibitisha usiri na unyamavu kuhusu maisha kingono ya siku za nyuma. Mizaha, dhihaka au hadithi kwa kujitetea kuhusu mapenzi au kondomu yaweza kuficha shaka na maarifa yenye kosa. Dhana za kiutamaduni kuhusu kiume zinatia wanaume mara nyingi moyo wa kufanya ngono na wenzi mbalimbali na kufanya wasiepuke kamwe bahati ya kutenda ngono. Laana ya ngono kati ya wanaume (mara nyingi inatazamia pia mapenzi kati ya wanaume na wanawake) inaweza kuzuia elimu sahihi kwa kufanya mahusiano hii kingono kuwa salama zaidi.

Jitayarishe vizuri kwa kutumia filamu. Tovuti ya filamu ina maarifa sahihi kuhusiana na VVU, UKIMWI na kondomu ambavyo vitaweza kukusaidia uwe tayari kwa maongezi muhimu kuhusu matumizi sahihi ya kondomu. Pia ina linki kwenye nyenzo ambazo zinaelekea vitendo katika mkusanyiko kwa ajili ya kuhusisha vijana na wanaume katika masuala yanayohusu kiume, jinsia, ufahamu wa VVU na afya ya ngono. Ingia kwenye tovuti ya Sonke Gender Justice.

Dokeza masuala ili watu wapate kuizungumzia na marafiki au katika familia zao baadaye, au kuifikiria kwa ajili ya mkutano ujao.

Inawezekana watu binafsi wawe waathirika wa VVU kwenye mkutono. Zungusha namba ya simu ya msaada, habari inayohusiana na ushauri nasaha miongoni mwa washiriki wote.

**Masuala ya majadiliano kuhusu filamu nzima**

Jinsi gani maisha ya watu katika filamu imeathiriwa na VVU au UKIMH?

Jinsi gani mtu huweza kutoshelezwa kingono wakati anapokua akijizuia kuambukiza na kuambukizwa VVU?

Mtu kwenye mkutano anauliza: *Kwa nini ikiwa kondomu zinapatikana VVU vinaendelea kuenea Afrika?* Mnawaza vipi?

Kwa nini ni ya muhimu kuelewa tofauti kati ya VVU na UKIMWI?

Jinsi gani kuwa na VVU siku hizi si hali gumu kudhibiti, na kuwa salama? Unafahamu watu wanaishi vema na VVU? UKIMWI umewahi kutisha maisha ya wamoja wao? Jinsi gani VVU vinaweza kutisha maisha?

Unakubali mtazamo gani katika filamu kuhusu kondomu? Haukubali?

*"Asilimia kubwa ya wenye kuathirika sasa ni watu wenye kufunga ndoa".* Jinsi gani mwenendo wa vijana na wanaume unaathiri hili? Jinsi gani mnaweza kushauriana kuhusu anasa yenu wote kutokana na ngono na matumizi ya mpira katika mahusiano ya muda mrefu kimapenzi?

Amara anasema hawezi tumia kondomu na mwenzi wake kwa sababu *"zinatatiza"* na zinapoteza anasa ya ngono. Mnafikiria nini kwa hiyo? Matatizo au mitihani gani watu wanaweza kupata wanapotumia kinga?

**Matumizi sahihi ya kondomu** ni vipi?

Kondomu zinakua za muhimu: kama umeathirika na VVU? umetahiriwa? una wakati moja wapenzi mbalimbali?

Ni / itaweza kuwa sawa wewe utumie kinga? Nini yaweza kukusaidia ufanye hivyo?

Unaweza kujisikia uhuru, kama Moruti, kuzungumza na mpenzi wako au mkeo kuhusu ngono salama, kondomu, kuchukua vipimo vya VVU pamoja, kubaki salama, kutojamiiana kwa muda?

Wanawake wanapenda wanaume watumie kinga?

David, mvuvi, anasema: *Sisi wenyewe tunasambaza magonjwa. Tusiogope kuzungumzia VVU na kondomu*. Mawasiliano kuhusu VVU, ngono na kinga yaweza kuwa vigumu. Nini ingeweza kusaidia mawasiliano sahihi kati ya wanaume wadogo na wanaume wakuu kuhusiana na fanaka kingono? kati ya wanaume na wapenzi, wake wao?

Moruti ameshinda kwa ajili ya kugawa ufasiri, kutengeneza mbinu, nidhamu, ushirikiano na mawasiliano yenye kufariji kati ya wanaume. Jinsi gani nyinyi, kama wanaume, mnachukuliana wenyewe na vijana ili mupate kuwa na mahusiano salama na yenye

kutosheleza kingono, kuelewa na kuepuka VVU na musiwe na tatizo kuhusu njia za kukinga miili yenu?

Unaweza kutayarisha majadiliano kuhusu matumizi na upatikanaji wa kinga kwa ajili ya wanaume katika jumuyia yako?

**Masuala ya majadiliano: Sehemu ya Afrika ya Kusini**

George anafasiri ya kwamba “Zaidi ni vijana wana VVU”. Wotu wote umefahamu wenye VVU ni vijana? Ni umri au mtazamo inakuweka katika hatari?

Mkocha wa Moruti anasema “kupata VVU kutokana na kutojali katika kipindi kimoja cha mapenzi bila kinga huweza kuharibu shughuli ya manandondi na kumaanisha kwamba atakufa”. Unaweza kufasiria jinsi gani kuwa na VVU imekua **hali raisi** kumudu, ukichunga afya bora? Unajua watu wanaishi tayari na VVU? UKIMWI umewahi kutisha maisha ya wamoja wao? Jinsi gani VVU vinaweza kutisha maisha?

Kama unchukua vipimo na wewe ni muathirika wa VVU, wapi waweza kupata tiba ya ARV? Utatafuta msaada gani, toka wapi?

Kondomu zinakua za muhimu: kama umeathirka na VVU? umetahiriwa? una wakati moja wapenzi mbalimbali?

Unaweza kupoteza kazi yako kwa sababu umeathiriwa na VVU? Una haki gani?

Msimamo wa George ni kawaida kwako? Ilibidi azungumzie usalama wa ngono na vijana katika gym yake?

Binti wake anasema “kama mtu wa karibu ya George anafariki kutokana na UKIMWI, ataweza kuzungumzia VVU na kinga”. Lakini mila yake ya kienyeji inakuwa kikwazo kikuu zaidi? Kati yenu kuna ambae amewahi kuvunja mila yake?

Nini inaweza kusaidia vizuri mawasiliano kati ya wanaume wadogo na wakuu kuhusu raha ya ngono? Kati ya wanaume na wapenzi, wake?

Unaweza kujisikia uhuru, kama Moruti – kuzungumza na mpenzi wako au mkeo kuhusu ngono salama, kondomu, kuchukua vipimo vya VVU pamoja, kubaki salama, kutojamiiana kwa muda?

Jinsi gani mnaweza kushauriana kuhusu raha yenu wote kutokana na ngono na matumizi ya mpira katika mahusiano ya muda mrefu kimapenzi?

Mshindi wa dunia hana tatizo kuhusu maisha yake kingono, mara zingine kutofanya mapenzi kabisa. Mfano wake umetuonyesha nini?

Moruti anasema: “maandalizi yangu ya mwili na roho ni sawa: mimi ni tayari”. Watu wanaweza kuandaa vipi miili yao na roho zao ili waepuke au wamudu VVU ijapokuwa kuna vishawishi kingono toka matangazo, habari, biashara ya ngono, kuishi pamoja kwa ustarehe katika jamii, kunywa au maisha ya mabwalo?

Moruti ameshinda kwa ajili ya kugawa ufasiri, kutengeneza mbinu, nidhamu, ushirikiano na mawasiliano yenye kufariji kati ya wanaume. Jinsi gani nyinyi, kama wanaume, mnachukuliana wenyewe na vijana ili mupate kuelewa na kuepuka VVU, musiwe na tatizo kuhusu jinsi ya kukinga miili yenu, na mupate kugawa busara na wapenzi wenu, ili nyinyi nyote mupate faida?

**Masuala ya majadiliano: sehemu ya KENYA**

Jinsi gani maisha ya watu katika filamu imeathiriwa na VVU na UKIMWI?

*"kwa nini, kama kinga zinapatikana, VVU vinaendelea kuenea Afrika?" - "UKIMWI haujawahi kufasiriwa vizuri kwa watu, au kusema kama unatumia kinga waweza kuuzuia."* Neno hili ni halisi kuhusu vijana na wanaume umefahamu?

Kwa nini ni ya muhimu leo kuelewa tofauti kati ya VVU na UKIMWI?

*"Tusijidanganye wenyewew… Nususi ya mambo ni kwamba watu wanafanya mapenzi."* VVU vinaendelea kuenea. Jinsi gani twaweza kulinda mapenzi katika usalama?

*"Nimepoteza dada, kaka, mume kwa ukosefu wa ufaham. Wangelijua kuhusu kondomu wangelikua bado wapo."* Athari za kunyamazisha elimu ya kondomu, kusema vitu vibaya kuhusu kondomu na kukatisha tamaa ya matumizi ya kondomu zinakuwa vipi?

*"Asilimia kuu ya waathirika ni watu wenye kufunga ndoa."* Jinsi gani mwenendo ya vijana na wanaume inaathiri hii?

*"Elimu ya kondomu inathibitisha mahusiano ya ovyo kimapenzi"* Mzee moja anasema. Unakubali au haukubali? Miongoni mwa VVU, jinsi gani twaweza kuchanganya ufahamu pamoja na ufarisi na kuthibitisha thamani za kiadili? Kama unhubira adili za kikristu au za kiislamu – kutofanya ngono kabla au inje ya ndoa – lakini jinsi gani vijana na wanaume wanaweza kuvutwa ili wakubali kutumia kinga kama wana **fanya**?

Ulikuwa na mawazo gani kuhusu uaminifu na ushujaa wa askofu alipotoa ukweli kuhusiana na hali yake ya VVU?

*"aibu ndiyo imekatilia watu wetu mbali nasi."* Umezungumza wazi wazi na baba yako (mwanako) kuhusu VVU au umuhimu wa kondomu kwa ajili ya uzuiaji wa VVU na usalama wa ngono? Nini inaweza ikakusaidie ufanye hivyo?

Nini ambae vijana na wanaume wanahitaji kujifunza kuhsiana na kinga ili wapate kuzitumia kwa usahihi bila shaka lolote?

Unapokunywa vileo *"hauwezi kuvaa kinga kwa usahihi, unapata kizunguzungu na halafu unasema 'Mimi ni mwanaume, UKIMWI haupo' – na mwisho wake utafariki peke yako."* Suala la majadiliano!

Unahitaji kujiandaa juu ya kuhakikisha upatikanaji kuu wa king katika jumuiya yako?

Umewahi kushiriki katika mikusanyiko kuu ya raia kwenye jumuiya huko maoni tofauti inayohusiana na uzuiaji wa VVU imezungumziwa kwa ukweli. Yawezekana upange moja?

**Masuala ya majadiliano: sehemu ya SIERRA LEONE**

Imeandikwa katika mabango barabarani: **VVU yaweza kuzuiwa. Ila tu waweza kusimamisha UKIMWI na CHUKUA HATUA UPATE KUSIMAMISHA UKIMWI. JIPIMISHE LEO.** Mtu anaweza kuzuia VVU jinsi gani? Kwa nini inakua tatizo kuchukua vipimisho?

Nancy anamuambia mwanake: "*Inabidi hakika uelewe ina maana gani kuwa kijana mzuri ambae anakua*?

Na ya muhimu kwa vijana wadogo kuona watu wakubwa wakisema wanajikinga na VVU, au wanashughulika katika kuthibitisha raha kimapenzi na uzuiaji wa VVU?

Teeleema ana gadhabu kuhusu nidhamu za wazazi. Amara anaishi katika mazingira ya vijana huko mambo kama ufahamu wenye makosa, udenguaji na matendo ya ngono inaenda kinyume na thamani za babake. Kama nususi za jumuiya na pendekezo zinasukuma vijana mbali na mashauri ya watu wazima, *mbinu* gani itatosha kwa kuthibitisha afya na salama kimapenzi ya vijana?

Ingawa lengo nzuri, kuna mawazo mengine kuhusu ngono miongoni mwa vizazi vya mbele isiyosaidia vijana ambao wanaendelea kutetea maisha yao kiraia, kiuchumi na kingono katika ulimwengu wa siku hizi?

Amara anasema: *'Mimi sitaki shida lolote kutoke, kwa hiyo mimi situmie kinga na mmojawapo wa wapenzi wangu'*. Shida gani anamaanisha?

Mahali kinga zinapewa, vijana wanabeza kuhusu kujisifu kwa ajili ya ujasiri kingono. Amara na Marafiki wanacheka, wikihakikisha ngono ya ' mnofu kwa mnofu', wakikataa kondomu. Jinsi gani mtindo huu wa kutania kwa kiume unaathiri wanaume?

Mawazo gani isiyokuwa sahihi imetolewa na marafiki wa Amara na inawaweka katika hatari ya VVU?

Mpenzi wa Amara anacheza akitania kuhusu mabadiliko ya uja na kubaka. Una wazo gani kuhusu lile? Unafikiri dhana zenye kosa (kama vile imekua mara nyinga katika biashara ya ngono) zinaathiri mahusiano ya kingono?

Jinsi gani kumbukumbu na ghamu ya vita inaweza kuathiri mtazamo ya wanaume kuhusu matumizi ya kondomu na mapenzi?

Jinsi gani umaskini unaathiri mahusiano ya kimapenzi?

Wazo la Amara linabadilika anapokua na baba yake, akijifunza kuhusu hali yake, Shabaha zake, udhaifu wake na imani yake? Jinsi gani uzuiaji wa VVU unaweza kuhusikana na vipimo tofauti vya maisha ya wanaume (matumaini, ndoto) na kusongwa kutokana na kawaida ya jinsia kwa kuishi 'kama mwanaume'?

Baada ya vita na kupoteza maisha, kuna kusongwa na pendekezo kwa kupata watoto. Kinga zinaweza kusaidia afya ya ngono, afya ya mimba na zaidi kwa wenye kurudi katika kulea watoto? Jinsi gani kondomzitapata nafasi katika maisha ya wao wanaopenda kupata watoto?

**Maneno itajadiliwa kuhusu 'Maziada'**

**1. NJIA ZA MSAADA**

Kuhusu majadiliano:
Kwa nini Yohana hakufahamu haraka kwamba ana VVU?
Ingawa wao wawili ni wenye kuathirika na VVU, ingewezekana mwana wao hasiwe na VVU? Wangelijua hali yao ya VVU, nini ingeoneza kinga ya mtoto wao na VVU?
Kwa nini kutumia kondomu ikiwa unakunywa dawa ya ARV?
Kwa nini Yohana aliacha kunywa madawa yake ya ARV?
Jinsi gani kuwa na wapenzi wengi inaongeza hatari ya VVU?
Jinsi gani mume na muke wanaweza 'kukinga ngono yao salama' na kuhakikisha kwamba HIV isiingie katika ndoa yao'?

**2. SOMO LA KONDOMU KATIKA CAPE TOWN**

Kuhusu majadiliano:
Nini imekugusa zaidi katika majadiliano hii?
Kwa nini watu wanafanya ngono isiyo salama?
Wanaume wanalaumu kondomu bila kuwa na ufahamu sahihi kuhusu matumizi yake?
Kondomu zinatosha, kama zinatumiwa vizuri na kwa usahihi?
Kwa nini mafuta ni ya muhimu pamoja na kondomu wakati wa ngono na ngono kinyume?
Una hisi katika kondomu?
Bila kondomu, hakuna mapenzi?

**3. KONDOMU KAMA UNAJALI**

Kuhusu majadiliano:
Watu hawatumii kondomu kwa sababu zimeonekana kuwa kinyume na maadili. Lakini hili haliwazuie kufanya mapenzi.
Kama una ogo na soni, unaweza kutumia vibaya kondomu
Kama ni muathirika wa VVU, unaweza ukaishi maisha yenye kutosheleza kingono kwa kutumia kila mara kondomu.
Kondomu ni vifaa vya maisha kwa kila ambaye anatumia ngono.
Kondomu zinakupa raha moja moja kama 'ngono ya nyama kwa nyama'.
Wao ambao hawatumii kondomu wanaizungumzia maneno mabovu. Wao ambao wanazitumaia wnajua faida.
Wakati unatumia kondomu, mwanangu, unajifanyia hivyo mwenyewe, kama uwekezaji kwa kuishi muda mrefu katika wakati wenye kujaa na VVU... Ninasema hii kutokana na upendo kubwa ninao kwako.

**4. KAMA WANAUME… UHODARI WA KUBADILIKA**

Kuhusu majadiliano:
Nini wanaume wanaitaji kufanya ili wazuie kuenea kwa VVU?
Sababu madawa ya ARV inawezesha kuishi vizuri na VVU na inasaidia kuepuka UKIMWI, kwa nini kondomu zinakuwa za muhimu?
Wanaume wana aina gani tofauti ya mahusiano kimapenzi? Kondom zinahitajiwa kila mara?
Vijana na wanaume wanakosa ufahamu mara nyingi na msaada ya kitamaduni wanaoitaji kwa kuepuka VVU? Kama baba, mwana, kaka, rafiki, unaweza kuibadili jionsi gani?

**Tovuti ya KINGA: http://protectionthefilm.com**

Katika mtandao unaweza kugundua kuhusu filamu, kusoma ufupisho mambo yaliyomo, kuangalia sehemu fupi za filamu – na kujua jinsi gani kuagiza DVD. Waweza pia kupata toleo la hiki Kitabu cha Msaidizi linaloweza kupakuliwa katika mojwapo ya lugha 7. Unaweza kuona pia 'maziada' mane mafupi kwenye DVD – kwa matumizi katika mikutano mifupi – au majadiliano katika vikundi, marafiki na familia.

Utapata maelezo kuhusu VVU na UKIMWI; ufafanuzi wazi wa kondomu kwa juu ya wanaume, pamoja na mealezo kwa kinaganaga kuhusu matumizi sahihi; na hadithi ya VVU katika mazingira ya kiafrika huko ni lazima sasa wanaume na vijana wapate kujulishwa wazi wazi kuhusu kinga na kupewa uwezo wa kuzitumia katika tendo la ngono.

Kuna linki kwenye nyenzo zingine za kuthibitisha shughuli ya uzuiaji wa VVU – ambazo zinatumiwa pamoja na DVD au zenye kutengwa nayo. Hizi zinakuelekeza mara moja kwenye jumuiya, vifaa vya mbinu, nyenzo za elimu na machapisho, vijitabu pamoja na makala achana achana kwa kusaidia uchunguzi wa dhana kwa alili ya kushirikisha wanaume na vijana katika masuala ya jinsia, raha ya ngono na Afya ya uzazi.

**Sonke Gender Justice Network**
inatumika katika Afrika kwa kuthibitisha uwezo wa serikali, ushirika wa wananchi na wananchi ili hatua ipate kuchukuliwa kwa:
* kuthibitisha usawa wa jinsia,
* kuzuia udhalimu nyumbani na katika ngono, na
* kupunguza kuenea na kuathiri kwa VVU na UKIMWI.

Shughuli yake inasaidia maendeleo ya jumuiya huko wanaume, wanawake, vijana na watoto wanaweza kupata faida za mahusiano yenye kuwa sawa, bila tatizo na yenye kutosheleza ambayo inasaidia katika maendeleo ya jumuiya sawa ya kidemokrasia.
**Mtu mmoja anaweza kukampeni** inakua mradi wa muhimu zaidi wa Sonke.

**MenEngage**
ni muungano wa kimataifa wa shirika zisizo za kiserikali na shirika za Umoja wa Mataifa ambayo inakusudia kuingiza vijana na wanaume katika njia sahihi za kutekeleza usawa wa jinsia na kuthibitisha afya na raha ya wanawake, wanaume na watoto.

**Mradi huu umefadhiliwa na Shirika la Ushirikiano wa Maendeleo la Norway (Norad), pamoja na msaada kubwa toka Baraza ya Wakimbizi ya Norway.**